# TCCIA INVESTMENT PLC

## TAARIFA YA MKUTANO MKUU WA KUMI NA SABA

**Tunapenda** kukujulisha kuwa **Mkutano Mkuu wa Kumi na Saba wa Wanahisa wa TCCIA Investment PLC**, utafanyika siku ya **Jumamosi** tarehe **5 Novemba 2022**, kwa njia ya mtandao. Mkutano utaanza **saa Tatu kamili (3.00) asubuhi**. Kampuni itawatumia Wanahisa wote kupitia simu zao za mkononi utambulisho na maelekezo kuhusu jinsi ya kujiunga na kushiriki Mkutano Mkuu kidijitali.

**Dondoo za Mkutano Mkuu wa Kumi na Saba ni:**

1. Kufungua Mkutano Mkuu wa Kumi na Saba;
2. Kupokea na kuridhia Dondoo za Mkutano Mkuu wa Kumi na Saba;
3. Kuthibitisha Kumbukumbu za Mkutano Mkuu wa Kumi na Sita;
4. Kupokea, kujadili na kuridhia utekelezaji wa Maazimio ya Mkutano Mkuu wa Kumi na Sita;
5. Kupokea, kujadili na kuridhia Taarifa ya Wakurugenzi wa Bodi ya Kampuni na Taarifa ya Mahesabu yaliyokaguliwa kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 31 Desemba, 2021;
6. Kupokea na kuridhia pendekezo la Bodi kuhusu Malipo ya Gawio kwa Mwaka 2021;
7. Kupokea, kujadili na kuridhia pendekezo la Bodi kuhusu uteuzi wa Mkaguzi wa Mahesabu ya Kampuni kwa Mwaka wa Fedha unaoishia 31 Desemba, 2022;
8. Kupokea, kujadili na kuridhia pendekezo la Bodi kuhusu Malipo ya Wajumbe wa Bodi;
9. Kupokea, kujadili na kuridhia pendekezo la kampuni kununua baadhi ya hisa zake (share buyback);
10. Kupokea na pendendekezo kuorodheshwa hisa za kampuni kwenye soko la hisa la Afrinex-Mauritius (Cross-Listing);
11. Kupokea, kujadili na kuamua mapendekezo kutoka kwa Wanahisa;
12. Kufunga Mkutano Mkuu wa Kumi na Saba.

**Maelezo:**

1. Mapendekezo yote kutoka kwa wanahisa yatakayojadiliwa katika dondoo namba 11 yatumwe na kumfikia Katibu kabla tarehe 25 Octoba, 2022.
2. Taarifa ya Mwaka 2021 na Makabrasha ya Mkutano yatapatikana kwenye tovuti ya Kampuni *(https://www.tcciainvestment.com)* kuanzia tarehe 25 Octoba, 2022.
3. Endapo Mwanahisa atashindwa kuhudhuria anaombwa kuteua Mwakilishi atakayehudhuria mkutano kwa niaba yake. Fomu ya Uwakilishi inapatikana kwenye tovuti ya Kampuni *(https:// www.tcciainvestment.com)*. Fomu za Uwakilishi zilizojazwa zitumwe kwa Katibu kupitia barua pepe info@tcciainvestment.com au picha ya fomu ya uwakilishi iliyojazwa itumwe kwenye WhatsApp na +255 684 535 545 na kumfikia Katibu kabla ya tarehe 3 Novemba, 2022.
4. Wakurugenzi wamependekeza ulipwaji wa gawio la shilingi 10.

**Tarehe za kuzingatia:**

**Tarehe ya tangazo:** - 19 Septemba 2022
**Hisa kuuzwa pamoja na gawio:** - 19 Septemba 2022
**Mwisho wa hisa kuuzwa pamoja na gawio:** - 6 Octoba 2022
**Hisa kuanza kuuzwa bila gawio:** - 7 Octoba 2022
**Daftari la wanahisa kufungwa:** - 11 Octoba 2022
**Malipo ya gawio kwa Wanahisa:** kuanzia tarehe - 7 Novemba 2022

**Imetolewa kwa niaba ya Bodi ya Wakurugenzi.**

**Peter W. Kifunguomali**
**Katibu**
20 Septemba 2022